MAZUNGUMZO YALIYO NYOFU KUHUSU
KUZALIWA MARA YA PILI
Na KUBATIZWA

Na

Lenta Hall

Kamiah, Idaho, USA 83536

MAZUNGUNZO YALIYO NYOFU KUHUSU KUZALIWA MARA YA PILI na KUBATIZWA

Majibu na maswali yenu kuhusu kupata uwokovu.

Na

Lenta Hall

ISBN:

Kitabu kimechapishwa katika nchi ya Amerika

Toleo la kwanza 1999, Toleo lilo sahihishwa nakala 2003

Mtengezajina mwandishi, Lenta Hall

Pich na Lenta Hall

S. L. P. 731, Kamiah, ID 83536

Simu: 208-935-0602

Burua Pepe: Lenta53@myfam.com

Haki za mwandishi

Haki zote zimehifadhika. Nakuna sehemu ya hiki kitabu yaweza kipigwa chapa mfano huu au kupisha katika mfano wowote au namna yeyote, kutumia umeme aukufanyika kwa mashine, pumoja na kutoa nakala, kufunasisha, au kula namna yeyote kwa mtambo wa akiba na wakurudisha tena, bila ruhusa ya barua kutaka kwa mtoa vitabu.

Mamna tafsili ya Biblia ingine, ila ya mfalme yakobo yaweza kutumiwa kunukulu maandiko matakatifu katika kitabu hiki.

UTANGULIZI

Ushuhuda Wangu

Nilipo keti chini ya msunobari (MTI) katika mkutano wa kituo cha Biblia cha Montana, Wachungaji Johnny Barkman na Sam Gupton walikuwa wana hubiri. Nilikuwa sijawai kuwa kanisani, ili onekana walinena katika lugha geni. Lazima ni “zaliwe mara yapili”, “Yesu alinipenda”, “mwanawe wa pekee”, “Yesu alinipenda”, “baptizweni” na mahubin yakaendalea, na kuenduea.

Usiku mmoja wakati wa huu mkutano Johnny alisimama na kueleza jinsi Yesu a natupenda na tulihitaji kuomba a ingie miyoni mwetu. Nalikuwa sijawaii kusikia kuhusu Yesu. Yote niliyoyajua ni Mungu peke yake, aliye mkubwa na mkali, katika mbingu, ambaye atatupa kuzimuni kwa ajili ya tabia mbaya au kutupeleka Mbinguni iwapo tunaweza kujali amri za kikristo. Basi tayari nalijua ni jinsi gani nalikuwa mkamilifu, katika nia, kuenda Mbinguni halikuwa ndilo Swala.

Nina huyu Yesu, a nayezungumziwa? Na ni vipi dumiani hapa alinifilia mimi? Ni vipi ulimwengu akaenda umbali huu? Na vipi duniani angependa mtu kama mimi kiasi hicho? Maswali haya yalipiga mizinga nia na moyo wangu.

Usiku wa juzi katika hema la kikundi chetu, naliuliza yule msichana niliyekuja naye anielezee mambo hayo.

“Nieleze wewe hii, isikuwe habari mzito kwako” msichana akesema nalikuliza uje nami kwa sababu Mama yako alitaka mtu wakuja naye kunijunguza. Msichana huyo akapaliza sauti kutoka chini lahilo hema na akaondoka kuelekea mahala pasipo fahamika…… Nika Zirai, nika udhika, aah nikavunjika. Yale Johnny alisema yali amsha njaa ambayo haingeweza kuondolewa kwa maneno yake.

Usiku uliofuata Johnny alizungumza kuhusu toba na uwokovu “Unahitaji kuokoka, kutubu dhambi zako na Yesu aingie moyoni mwako” Akaongeza, Yesu atasamehe dhambi zetu na kuokoa kuto ingia kuzimu. Na sasa lile neno kuzimu nalifahamu, sasa nikafikiri, na nikaona sitaki kuenda kuzimu.

Nalitaka niende mbele ni “okoke” alicho maanisha na haya yalinihofisha, magoti yangu yakatetemeka nilipo anza kuenda mbele.

Kilicho fuata ni kubadilisha maisha yangu hata milele. Johnny alitu fanya tuka piga magoti huku akituongoza katika ombi fupi ya kumkubali Yesu Kristo kama Bwana wa maisha yetu. Alitu ambia tuli mhitaji kumwomba atu samehe dhambi zetu na kwamba alikuwa amehaidi kufanya hivyo.

Hakukuwa na namna ya kueleza kilicho tukia ndani mwa nafsi yangu, ila nikusema Yesu alinipata pale nikipiga magoti kwa sakafu ya musonabari katika vilima vya Montana.

Kulikuwa na waliopiga magoti kama kumi na tano au ishirini, walio enda mbele, na tukagawanywa katika makundi madogo na kuelekezwa na washauri, ambao walitueleza zaidi ya chaguo la maisha mapya. Tukapewa kitabu kidogo “Sasa ninapo Amini” ambacho ningali nacho mpaka sasa.

Yule mshauri wa kikundi changu, Becky, aliyaeleza hayo maneno geni na akapitia kikamilifu katika Biblia yake akituonyesha mistari zaweza kupatikana wapi.

Kurudi katika hema, karibu katikati mwa usiku, nili endelea kuuliza mswali mpaka mwishowe nika-ambiwa niende nilale.

Kuzaliwa tena kiroho imedumu miaka mingi. La, bado sija kuwa mkamilifu, nerudi nyuma wakati mwingine, lakini Mungu ameendelea kuwa mwanifu, akinitia nguvu, akiniita tena nilipo potoka, na sasa naweza kutambua njia mbaya na nidumu kwa nehema katika njia na mapito yake.

Kitabu hiki ushikacho mikononi kitaeleza Kuzaliwa mara ya Pili, manna yake, kita kacho tukia na mengi zaidi. Mungu ni kweli. Uhusiano na yeye hauwezi kubadilishwa na vitu ambavyo ulimwengu waweza kutoa.

Basi na Ubarikiwa unapo soma na ufikie ufahamu Wake Na Neon lake. Kama una maswali unakaribishwa kuniandikia au kutuma barua pepe (email) kuna anuani zingine nyuma ya kitabu pia na nambari za simu.

Maombi yangu yawajia kwa kila moja wenu achukuwaye na kusoma kitabu hiki. Na omba unpokea Yesu Kristo kama mwokozi na uje katika kundi. Nitapenda kusherekea nawe siku moja Mbinguni.

Lenta

YALIYO NDANI:

UKURASA WA HAKI YA MWANDISHI

UTANGULIZI: Ushuhuda Wangu

ZUNGUMZO NYOFU 1

UFAFANUZI WA MASHARTI YA KUZALIWA MARA YA PILI 4

AMINI 4

KIRI 5

TUBU 6

OMBA, TAFUTA NA POKEA 9

MSAMAHA 10

UBATIZO WA TOBA (MAJI) 14

UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA MOTO 16

MFANO WA MAOMBI 18

MAISHA YETU MAPYA 19

SISI NI AKINA NANI KATKA KIRISTO 19

NI KITU KIPI TUNACHO AMINI 20

MAE LE KEZI YA YESU KUKUSU MAISHA YA KIKRISTO 21

AMRI MBILI KUUZA YESU 25

KATIKA TAMATISH NENO LA MWISHO 25

KUSHIRIKI HABARI NJEMA ULIZONAZA 26

MAZUNGUMZO YALIYO NYOFU KUHUSU KUZALIWA MARA YA PILI NA KUBATIZWA

Maswali na Majibu Toka Biblia

Nime uliza mara nyingi, katika makundi Nimeyafundisha, yamaanisha nini Kuzaliwa Mara ya Pili? Hook wengi wali ambiwa wakaribishe Yesu ndani ya moyo wao Hawa kuwa na ufahamu timilifu kwa nini wamkaribishe **Yesu dani yao au mabadiliko yapi, yange tukia maishani mwao baadaye.**

Ubarikiwa upya na ufahamu maalumu wa Bwana na Mwokozi wetu unapo soma kurasa hizi.

KUZALIWA MARA YA PILI HAKUWEZI KUIMARISHWA TU KWA SAFU, WALA TARATIBU ZA UTII. LAKINI NI USTADI WA UZOEFU, wa kumfikia Mungu wa Mbinguni kupitia Yesu Kristo, mwanawe, yaani kuimarisha uhusiano uliovunjika kwa ajili ya dhambi ya Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni.

(Maneno mengi hutumiwa kueleza neno kuzaliwa mara ya pili: Kama – Ni – Kukombolewa, kuokoka, kuzaliwa mara ya pili, kuzaliwa upya, kuongoka n. k. a.)

Hapo papo tufikapo ufahamu jinsi neno la Mungu lasema kuhusu kuzaliwa mara ya pili ndipo tuakabiliana na-haguo. Je twaweza kubali thamani ya kweli yake na kufanya Yeye awe Bwana wa maisha yetu? Je twaweza kumkata na kushikilia sanamu ya ulimwengu huu, Lucifa (Shetani) kama bwana wa maisha yetu? **Umilele wa siku za usoni wategemea chaguo tunalolifanya. Kuna barabara mbili ya hiari yako.**

Je Ina Tupasa Kuzaliwa Mara Ya Pili?

Yesu asema tusipo Zaliwa Mara Pili hatuwezi kuingia katika ufalame wa Mungu.

Yohana 3:5-7

5. Yesu akajibu, Amin, amin, nakumbia**, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu**.

6**. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, kilichozaliwa kwa Roho ni roho.**

7. Usistaajabu kwa kuwanilikumbia, **Hamna budi kuzaliwamara ya pili**.

Marko 8:36

Je, kuna faida gani mtu kuupata ulimwengu wote na kuyapoteza maisha yake?

Ni Ipi Hali Yetu Kabla Kuzaliwa Mara Ya Pili?

Tokea wakati wa kuunguka kwa Adamu katika dhambi wazao wake wote wamezaliwa na mbegu ya uovu idumuyo ndani mwao. Ambayo ilikaribia mbegu ya utakatifu. Matokeo ikawa makao ya asili ya dhambi ambayo mwandamu anahitaji kukombolewa toka kwayo, au afunguliwe. Hii ili komesha ruhusa yetu ya kuingia Mbinguni na ikaharibu utakatifu wetu.

-

Warumi 3:23

23. Watu wote wametenda dhambi na wamepungukiwa na utukufu wa Mungu;

Warumi 5:12, 10-11

12. Kwa njia **ya mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, nayo ikasababisha kifo; Kivyo kifo kimeenea katika jumuiya yote ya binadamu, kwa maana wote wametenda dhambi.**

10. Maana, tulipokuwa bado adui zake, **Mungu alitupatanisha naye kwa kifo cha Mwanae**. Na kwa vile sasa tumepatanishwa naye, ni **dhahiri zaidi kwamba tutaokolewa kwa uzima wa Kristo**.

11. Wala si hayo tu, ila tunafurahi pia katika Mungu **kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo ambaye ametupatanisha na Mungu.**

Ni Vipi Baba Wa Mbinguni Hutuona Kabla Tujazaliwa mara ya pili?

Mungu anataka upatanishi wa viumbe kwake mwenyewe.

Warumi 5:8

8. Lakini **Mungu amethibitisha kwamba anatupenda, maana wakati tulipokuwa bado wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.**

I Timotheo 2:1-6

1. Kwanza kabisa, **basi, naomba dua, sala, maombi na sala za watu wote**,

2. Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, ili tupate kuishi maisha ya utulivu na amani pamoja na uchaji wa Mungu na mwenendo mwema.

3. **Jambo hili ni jema na lampendeza Mungu Mwokozi wetu**,

4. **Ambaye anataka watu wote waokolewe na wapate kuujua ukweli.**

5. Maana **uko Mungu mmoja, na pia uko mmoja anayewapatanisha watu na Mungu, binadamu Kristo Yesu,**

6. Ambaye alijitoa mwenyewe kuwakomboa watu wote.

Luka 19:10

10. Kwa maana **Mwana wa Mtu amekuja kutafuta na kuokoa waliopotea**.

1 Yohana 4:9-10

9. **Na Mungu alionyesha upendo wake kwetu kwa kumtuma Mwanae wa pekee ulimwenguni, ili tuwe na uzima kwa njia yake.**

10. **Hivi ndivyo upendo ulivyo; si kwamba sisi tulikuwa tumempenda Mungu kwanza, bali kwamba yeye alitupenda hata akamtuma Mwanae awe sadaka ya kutuondolea dhambi setu**.

Yeremia 29:11

11Maana **nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA,ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho**.

Yesu anaeleza sharti la kuzaliwa mara ya pili:

Yohana 3:1-10

1. Kulikuwa na kiongozi mmoja Myahundi, wa kikundi cha Mafarisayo, jina lake Nikodema.

2. Siku moja alimwendea Yesu usiku, akamwambia, “Rabi, tunajua kwamba wewe ni mwalimu uliyetumwa na Mungu, maana hakuna mtu awezaye kufanya ishara unazozifanya Mungu asipokuwa pamoja naye.”

3. **Yesu akamwambia**, “Kweli nakwambia, **mtu asipozaliwa upya hataweza kuuona Ufalme wa Mungu:**

4. Nikodemo akamwuliza, “Mtu mzima awezaje kuzaliwa tena? Hawezi kuingia tumboni mwa mama yake na kuzaliwa mara ya pili!”

5. Yesu akamjibu, “Kweli nakwambia, **mtu asipozaliwa kwa maji na Roho hawezi kamwe kuingia katika Ufalme wa Mungu**.

6. **Mtu huzaliwa kimwili kwa baba na mama, lakini huzaliwa kiroho kwa Roho.**

7. Usistaajabu kwamba nimekwambia kuwa ni lazima kuzaliwa upya.

8. Upepo huvuma kuelekea upendako; waisikia sauti yake, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda. Ndivyo ilivyo kwa mtu aliyezaliwa kwa Roho.”

9. Nikodemo akajibu, akamwambia,Yawezaje kuwa mambo haya ?

10.Yesu akajibu, akamwambia, Je! wewe u mwalimu wa Israeli na mabo haya huyafahamu?

Nikodemo alikuwa kiongozi wa dini katika Israeli. Alikuwa mwanasheria, wa uzao kamilifu na Elimu yake, na bado hakuwa na uwezo wa kuzaliwa mara ya pili katika roho. Yesu alimweleza kuzaliwa upya sio kazi ya nje ya mwili bali ni ndani mwake yaani ndani mwa roho. Ali mwambia mpaka azaliwa mara ya pili au hawezi kuona ufalme wa Mungu mwisho mwa maisha yake ya ulimwengu huu.

Mara nyingi tuafikiri kuwa Ukristo ni kutii mambo ya mwilini na sheria za kiroho katika Biblia. Tunafikiri kuwa ukristo ni kama kazi ya kawaida; kujaribu namna yetu kuenda Mbinguni. Badala yake, **ni Uhusiano Ulioyo imarishwa na Bwana.** Tuna anza kufata sheria namaagizo, sio kwa sababu ni lazima, bali tuna tamani kumjua na kumpendeza, na jinsi Yeye atamani sisi kumjua na tuwe watu wake. Kuna kitu cha kilindini, cha thamana, na uzoefu wa jazi uliopo kwa ajili yetu, ambayo hutuleta karibu na moyo wa Mungu, cha gusa nafsi na roho, na kuleta nguvu na uponyaji maishani mwetu.

Kunayo njia ya kipekee ya kutufunya kufikia uhusiano na Mungu. Ni kufuata Mpango wake wa uwokovu: yaani Kuzaliwa Mara ya Pili

Ili kwamba tufahamu umuhimu Mungu anahutiaya juu ya kuzaliwa mara ya pili, tunahitaji kujua ni kipi kipawa cha ajabu ametoa kwa niaba yetu ili tufikie. Ametutolea mwana wake wapekee.

Yohana 3:16-17

16 Maana Mungu aliupenda **ulimwengu hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee**, **ili kila amwaminiye** asipotee, **bali awe na uzima wa milele**.

17 Maana Mungu hakumtuma **Mwanae ulimwenguni ili** auhukumu **ulimwengu**, **bali** aukomboe **ulimwengu**.

Mwanadamu anahitaji la kipekee kumjua Mungu katika uhusiano wa kipekee Jinsi anaeleza katika Mathayo 7:21-23 (Tazama mistari hizo chini yake)

Jinsi tulivyo ona Katika hadithi ya Nekodemo, Mungu huyu ajuaye ni ufahamu unaotakana na Kuzaliwa Kiroho. Sio wote, na hata wote waliotenda maajabu Katika Jina la Yesu, wata urithi uzima wa milele. Ni wale tu **wanao Mjua Yeye na Wanatenda Mapenzi yake wata Urithi,** ndio **wanaotii Amri zake.**

Yesu alilipa gharama ya uwokovu wetu alipokufa Msalabani. Akawa ufunguo kwetu kuingia lango la mbinguni. Nasi sote tutasimama mbele zake, wote watakatifu na wasio okoka, wakati wa ufufuo utakapo fika. Tusipo zaliwa mara ya pili hatutaweza kuingia katika lango la mbinguni. Tusipo mjua tuta ambiwa Ondoka Kwangu Sikujui.

(Tafadhali nukulu: “'Kuna tofauti kati ya Utii na Uhalalisho ambao unasababisha ghasia na ugomvi katika ulimwengu wa Kikristo. Kama Wakristo tunatii amri za Mungu maana tuna moyo wakumpendeza. Iwapo tunatii sheria peke yake, tuna soma kwamba yatupasa au kwa sababu mtu anasema Lazima tufanye hili au lile ndio tufike mbinguni, hapo inakuwa uhalalisho. Utii wetu wafanywa vivi hivi, kwa kukata shauri, lisio toka moyoni halitufaidi lolote ila kuumwa na moyo: Mwili, yaani inje ya moyo ha uwezi kumpendeza Mungu. Tunaweza mpenda na kutii yeye iwapo mioyo zetu zimegeuzwa ndani yake na uhusiano wetu umeimarishwa na yeye. Basi shauku la moyo wetu litakuwa ni kutii sheria zake na kumpendeza yeye.”

Mathayo 7:21-23

21. **Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni**.

22.**Wengi wataniaambia** siku ile, Bwana, Bwana, **hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?**

23. Ndipo **nitawaambia dhahari, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu**.

Warumi 14:10-12

10. Lakini wewe je! Mbona wamhukumu ndugu yako? Au wewe je! Mbona wamdharau ndugu yako? Kwa maana **sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.**

11. Kwa kuwa imeandikwa, **Kama niishivyo, anena Bwana, kila goti litapiwa mbele zangu; Na kila ulimi utamkiri Mungu**.

12. Basi ni hivyo, **kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.**

Yohana 10:7-9

7. **Basi Yesu aliwaambia** tena, Amini, amin, nawaambieni, **Mimi ndimi mlango** wa kondoo.

8. Wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi: lakini kondoo hawakuwasikia.

9. **Mimi ndimi mlango**: mtu akiingia kwa mimi, ataokoka, ataingia na kutoka, naye atapata malisho.

Yohana 14:6

6. **Yesu akawambia**, **Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.**

UFAFANUZI WA MASHARTI YA KUZALIWA MARA YA PILI

-

Njia ya uwokovu ni rahisi. Lazima tukubali yale Neno la Mungu linasema kuhusu Yesu, tuliamini, na tumtafute. Yafuatayo ni maelezo ya kila sharti linalotumiwa kueleza Kuzaliwa Mara ya Pili.

1. AMINI

Ili uzaliwa mara ya pili lazima uamini moyoni mwako kwamba Yesu Kristo hakika alikuja kuokoa wewe. Moyo, Katika Bibilia, yamaanisha mambo ya katikati mwa kuwepo kwako; moyo wako, nafsi, na roho. Ha uwezi kutegemea hizia zako ambazo zimejawa makosa na si zakutegemea. *Ni moyo ulioandiliwa upya kwa Roho wa Mungu unaoweza kuamini Mungu licha ya hali zinazo uzingira. Jambo la ajabu kwa yote ni kwamba mtu wowote amtafutaye* anaweza kufanywa upya. Alikuja ili WOTE wa okoke. Yeye anawaita, anawakokota na hutafuta mwanadamu. Ni kwetu sisi kuitikia. Ni shauri unalokata kibinafsi. Uhusiano wa siku zetu za usoni hutegemea uchaguzi wetu.

Warumi 10:9-10

9. Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na **kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.**

10. Kwa maana **kwa moyo mtu huamini hata kupata haki; na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.**

Matendo ya Mitume 4:12

12. **Wala hakuna wokovu katika jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewakwalo.**

Yohana 5:24

24. Amini, amini, nawaambia,**Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini** yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumu, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.

2. KIRI

Kukiri kupo aina mbili.

Kukiri kwa **KWANZA** huja wakati tunapo jifunza kuamini ndani yake Yesu Kristo. Hufanya maneno ya masikizano, kupitia maombi, kufanya agano na Baba kwamba hakika, tuamini Mwanawe Yesu Kristo.

Kukiri kwa **PILI** hufanyika katika matembezi ya kila siku kwamba tumkubali Mungu katika yote tutendayo na tusemayo. Kukiri kwa kila siku kila neno litokalo vinywani mwetu.Je latoka kwa Mungu? Je laeleza Maoni yake, hata kama hatuhitalafiani na ulimwengu ulio karibu nasi?

Je Mazungumzo yetu ya kawada ya kila siku katika ulimwengu huu yamkubali yeye kama Bwana na Mwokozi ? *Iwapo Twamficha na hatukubali Uwepo wake maishani mwetu hapo tunamkana.* (Mathayo 10:33 Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.)

Je walio karibu nasi wamjua kwa mazungumzo yetu ya haki kwamba yeye ndiye kiini cha maisha yetu?

Tunapo nena toka Moyoni, je ni moyo uliojawa na Upendo na imani katika Kristo Yesu, au ni mng'ao wa mwengu unao tuzingira, ukiwa na uchungu, wivu na chuki?

Warumi10:10

10.Kwa **maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu**.

Warumi 10:9-10

9. Kwa sababu, **ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka.**

II Yohana 1:7

7. Kwa maana **wadanganyifu** wengi wametokea duniani, **wasiokiri ya kuwa Yesu Kristo yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo.**

****

Mathayo 12:34-37 (Yesu yuazungumza).....kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake.

35. Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema: na mtu mbaya katika akiba hutoa mabaya.

36. Basi, nawaambia, **Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.**

37. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.

Mathayo 5:37

37. Bali **maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo, siyo: kwa kuwa yazidiyo hayo hayo yatokakwa yule mwovu.**

Mathayo 10:32-33

32. Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni.

33. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.

Luka 12:8

8. Nami nawaambia, **kila atayenikiri mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri yeye mbele ya malaika wa Mungu:**

I Yohona 4:15

15. Kila akiriye ya kuwa Yesu ni Mwana Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu.

3. TUBU/ TOBA

Tubu ya maanisha nini? Yamaaninsha Kugeuka toka dhambini, yaani kukana, kuchukia dhambi, Jinsi Mungu ana chukia dhambi, kutayarika kwa ajili ya dhambi.

Mungu anatuamurisha kuchukia dhambi, jinsi anavyo chukia, **Tambua (**Lazima hii ni kuchukia dhambi tukumbuke sio kuchukia mtu atendaye dhambi, <u>hata kama yule mtu ni wewe</u>.)

Warumi 12:9

9. Pendo na lisiwe na unafiki **lichukieni lilo ovu**; mkiambatana nalilo jema.

I Petro:3:10-11

10. Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila.

11. **Na aache mabaya, atende mema**; Atafute amani, aifuate sana.

Zaburi 45:7

7. **Umeipenda haki**; **Umechukia dhuluma.**

Kwa hiyo MUNGU, Mungu wako, amekupaka mafuta, mafuta ya furaha kuliko wenzako. Ni lazima tufike mahala halisi ambako dhambi yaweza kufanyiza huzuni wa Uungu ndani mwetu, Kusikitikia dhambi zetu na matendo yetu mabaya.Tunapo jifunza toka kwa Mungu na kuwa ndani mwake, atatufunilia kwetu aina ya dhambi iliyopo Maishani mwetu. Neno lasema **naweza kufanya mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu.** (I Petro 4:13) na tena**, Hakuna Jaribu lilowapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu, ila Mungu ni mwaminifu, ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo, lakini pamoja nalile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. (I Wakorintho 10:13)**

Hizi mistari hazija toa ruhusa au msamaha wa kuwa wavivu na kutarajia Mungu kutupa Safari ya bure kuenda mbinguni. Hizi mistari ni himizo la kumtafuta wakati tunopo kuwa chini ya majaribio na mitihani, ili kwamba tukakuwe katika nguvu ndani Mwake. Mwili huu Utashindwa tukijaribu kufanya kwa Uweza wetu. Ina gharimu Nidhamu upande wetu. Tunapo chagua kutii sheria zake na kuishi kwa haki, na kumtafuta kwa ajili ya nguvu zetu kupitia Maombi, ndipo anaweza kubariki jitihada letu.

2 Wakorintho 7:9-10

9. Sasa **nafurahi**, si kwa sababu ya ninyi kuhuzunishwa, bali kwa **sababu mlihuzunishwa**, hata mkatubu. Maana mlihuzunishwa kwa **jinsi ya Mungu**, ili msipate hasara kwa tendo letu kaitka neno lo lote.

10. Maana **huzuni iliyo kwa jinsi ya** liletalo wokovu lisilo na majuto; **bali huzuni ya** dunia hufanya mauti.

Tunapo tubu dhambi zetu na moyo safi, Bwana naye huzifuta kutoka kwa hesabu yetu. Zaondolewa kwetu jinsi Mashariki ilivyo mbali na magaribi.

Zaburi 103:12

12. **Kama mashaki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.**

Ezekieli 18:20-22

20. Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayo kufa; mwana hatachukuwa uvo wa baba yake, wala baba hatauchukuwa uvo wa mwanawe, haki ya mwenye haki itakuwa juu yake, na uvo wake mwene uvo utakuwa juu yake.

21. **Lakini mtu mbaya akighairi, na kuacha dhambi zake zote alizozitend, na kuzishika amri zangu zote, kutenda yaliyo halali na haki, hakika ataishi, hatakufa.**

22. Dhambi zake zote alizozitenda hazitakumbukwa juu yake hata mojawapo; katika haki yake aliyoitenda ataishi.

I Yohana 1:9

9. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwanifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhulaimu wote.

Waefeso 1:5-7

5. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywa wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake .

6. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambaye ametuneemesha katika huyo Mpendwa.

7**. Katika yeye huyo, kwa damu yake tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake**

Wengi hukosa kuelewa Mstari huu ,lakini **Amri ya Mungu juu ya kila mtu na hali ya baadaye iliyopo hapa ya husisha kila MTU AMKUBALIYE YEYE. Mungu anataka kuturithi katika jamii yake. Yeye ame azimia mbele mwendo kwa wanao chagua kumfuta yeye. (Yeremia29:11** Maana nayajua mawazo ninayowawazia nyinyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, **kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.)**

Alimtuma Mwanawe kwamba WOTE wawe na nafasi ya kuokoka. Ni chaguo la kila mtu kufanya mwenyewe. Hakuna mtu anaweza kununulia mwengine huu urithi, wala waweza kutenda kazi haki kwa ajili yako**. (Zaburi 49:7** Hakuna mtu awezaye kukomboa ndugu yake, wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake.)

Hata wewe mwenyewe hauwezi kuipokea.Yesu tayari asha ilipia gharama ya kuzaliwa mara ya pili, alipo kufa Msalabani katika nafasi yetu. Hiki ni kipawa chake kwetu. Yeye ndiye Lango la pekee.

Marko 1:14-15

14. Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, **Yesu akaenda** Gililaya, **akiihubiri Habari Njema ya Mungu,**

15. akisema,Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia**; tubuni, na kuiamini Injili.**

Matendo Ya Mitume 3:19-21

19.**Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipatekuja nyakati zakuburidishwa kwa kuwako kwake Bwana;**

20. apate kumutuma Kristo Yesu mliyewekekewa tangu zamani;

21. ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.

Tafadhali tambua hapa kuna hatua mbili katika mstari huu:

1**. Tubu, au,** geuka toka dhambi ulizotenda kwa huzuni.

2. Hapo uta **Ongoka**. Hapo tu ndipo Mungu ananza kazi yake ndani mwako akikusababisha kuwa na nguvu za kukoma kutenda dhambi. Hapo uta kuwa tayari kwa ajili la buriidko lake.

Neno " BURIDIKO" ---- lamaanisha: Kuchangamsha kwa Roho wa Mungu tena.

Tulipo umbwa wakati wa kwanza tulijazwa na, natukazingirwa na utukufu wa Mungu na Roho wake. Hapo hakika tuliumbwa katika Mfano wa Mungu, katika Usafi na utakatifu na tukiwa na uwezo wakutembea katika Wepo Wake. (Mwanzo 1:27 **Mungu akaumba mtu kwa mfano wake**, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke, aliwaumba). Na (Mwanzo 2:19 **Bwana Mungu** akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, **akamletea Adamu** ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likiwa ndilo jina lake). Angalia hapa jinsi Adamu waziwazi anatembea na Mungu akiwaita wanyama majina.

Wakati Adamu na Hawa walipo anguka, usafi wa wanadamu, mfano wa Mungu na uweza wa kutembea katika wepo wa Mungu ukapotea. Ni katika hali ya Kuzaliwa Mara ya Pili ndipo tutakapo rudi katika Uhusiano ulio sawa na Mungu Baba. Nasi twafanywa Upya na kuumbika tena safi Kiroho na Roho wake. Roho huja kwetu, hungia hekaluni mwake, ambalo ni mwili wetu, na hufanya makao pale, akitufanya upya, akichangamsha na kutusafisha sisi tena.Utukufu wake mara ingine ujaza hekalu letu.

2 Wakorintho 6:16 Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? **Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.**

Wakati Mtu anapo tubu katka kweli, Mungu ataondoa dhambi za huyo mtu na kuanza kuponya na kumrejesha Mtu huyo.

(Fahamu. Watu hawakui papo na hapo Wakristo wakamilifu na wa ajabu kwa sababu tuna wakati wa kujifunza.Wakati mwngi twashindwa na ni lazima tutubu, lakini YEYE: MUNGU NI MWAAMINIFU kwetu tunapo endele kua.Tunapo tubu katika kweli na kuutafuta uso wake.Yeye atatusemehe na kuturejesha katika Ushirika naye.)

Huyu ni Bwana wa ajabu namna gani. Hasemi ya kwamba nita toa tu baadhi ya dhambi ..... asema dhambi zote kwa pamoja. Hasemi, sita ingia hekalu hili..... kwamba hekalu hili lime angukia mbali ..... kwamba lime haribiwa zaidi..... kwamba halifai kwa wepo wangu..... badala yake, husema wo wote ajaye..... (Yohana 3:16 Mungu aliupenda ulimwengu jinsi hii, akamtoa Mwana wake wa pekee, bali **wo wote amwaniye asipotee apate uzima wa milele.)**

Ufunuo wa Yohana 3:19-21

19. Wote niwependao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe wa bidii, ukatubu.

20. Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami ntakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.

20. Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.

Matendo ya Mitume 17:30

30. Basi, zamani zile za ujinga **Mungu** alijifanya kama hazioni; bali **sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.**

Hatuwezi kuchakua Mungu hivi hivi na kuenda kwa matakwa ya njia zetu. Tunapo kuwa tume fika katika Elimu ya ufahamu wa Kweli, na tunapo jua njia ya kumpata Yeye. Tunalo chaguo. Je tuaweza kumwiitikia Yeye na Wito wake au tuta gueka na kuenda mbali na yeye, tukipotewa na wokovu wake.

Isaya 55:6-8

6. **Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu ya karibu**.

7. Mtu mbaya na ache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie BWANA, naye atamrehemu, Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa.

8. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA.

4. OMBENI , TAFUTENI NA POKEA

Kumtafuta Mungu ni kulitia Jina lake kwa bidii na moyo wako wote Twahitaji kumtafuta katika Maombi, tukitatua mioyo zetu, tukijitoa kwake, tukiwa na shauku la kumjua katika uhusiano wa kweli na sio katika Elimu ya kichwani.

Mathayo 6:33

33. Bali **utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.**

Mathayo 5:6

6**. Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibiswa.**

Mathayo 7:7-8

7. **Ombeni, nanyi mtapewa;tafuteni, nanyi mtaona, bisheni, nyanyi mtafunguliwa.**

8. kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa.

Fahamuni kwamba katika kila mistari hizi , kuna ahadi maalum, kwamba atapatakana kwa wanao mtafuta Yeye.

Zaburi 14;1-2

1. Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu; Wameharibu matendo yao na kuyafanya chukizo, Hakuna atendaye mema.

2**. Toka mbinguni BWANA aliwachungulia wanadamu, Aone kama yuko mtu mwenye akili, Amtafutaye Mungu.**

Tunapo jikwaa katika dhambi na kuanguka toka kwa NEHEMA YA MUNGU, Mungu asema hivi:

Yoeli 2:12-13

12. Lakini hata sasa, asema **BWANA, nirudieni mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea:**

13. rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkarudie BWANA, Mungu wenu: kwa maana yeye ndiye mwenye neema, amejaa huruma, si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema, naye hughairi mabaya.

Fahamu hapa kwamba angali anajita Mungu wetu. Hata kama tumeanguaka atuambia tumrejelea kwa hivyo hatuta mpoteza. Anataka sisi turejee na kumtafuta katika huzuni wa kiuungu na toba ya dhambi zetu. Tazama mstari tulio soma katika sehemu iliofundisha TOBA AU TUBU (II Wakorintho 7:10 Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.)

Isaya 55:6-8

6. **Mtafuteni BWANA, maadamu anapatikana, Mwiteni, maadamu yu karibu**.

7. Mtu mbaya na ache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie BWANA, naye atamrehemu; Na arejee kwa **Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa.**

8. Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA.

Kumbukumbu la Torati 4:29

29. Lakini huko kama **mkimtafuta BWANA, Mungu wako, utampata, ukimtafuta kwa moyo wako wote, na roho yako yote.**

Methali 8:17

17**. Nawapenda wale wanipendao, Na wale wanitafutao kwa bidii wataniona.**

Methali 28:5

5. Watu wabaya hawaelewi na hukumu; **Bali wao waishikao hushindana nao.**

Yeremia 29:11-13

11. Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

12. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza.

13. Nanyi **mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.**

5. MSAMAHA

Mungu ana makusudi kubwa anapo hitaji sisi kusamahenana.

Mwishowe, msamaha utuweka huru hata wao walio tutenda dhambi na walio tukwasa. Kutosamehe ni dhambi. (Marko 11:25 Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu, ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.)

(FAHAMUNI, Neno: awa / wezekana katika Mariko 11, Epu tujue ya kwamba sisi wenyewe twashikilia ufunguo uonyeshapo kama Mungu aweza kutusamehe. Ni chaguo letu. Yeye anatamani sisi tusamehe. Ana tuelekeza kusamehe wengi, kumfungua awe huru na kuweza kutusamehe nasi.)

Tunapo endelea kushikilia uchungu na kutosamehe ndani ya mioyo zetu dhidi ya wenzetu hapo, hatuwapendi wao na kusamehe jinsi Mungu ametusamehe sisi. Kama mzao aliye chaguliwa na Mungu na mrithi pamoja na Kristo lazima tuwe kielelezo cha Msamaha na upendo wake kwa watu wengi. Mojawapo wa maneno Yesu' alisema ya

mwisho kabla afe msalabani yalikuwa, Baba , wasemehe hawajui walitendalo (ona Luka 23:24) Alisema haya kuelekeza kwa walio kuwa wakisulubisha .

Baba wa mbinguni hakusema, huyu mtu ametenda dhambi mbaya na siwezi kumsamehe. Alisema, Dhambi zenu zijapokuwa nyekundi sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. (Isaya 1:18 Haya njoni, tusemezane, asema BWANA: dhambi zenu zijapokuwa nyekundi sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa yekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.)

Kristo alikufa ili WOTE waweze kuokolewa, hata waliojiona kutopendwa, kutofikiwa. Lazima tuwe na nia ile ile aliyekuwa nayo kuelekea wengine. (I Wakorintho 2:16 Maana ni nani aliye fahamu nia ya Bwana, amwelimishe? **Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.**) Nia yake ilikuwa ni ya kusamehe na wokovu kwa wote watakao mpokea.

Wengi wetu tumepitia dhambi ambazo hatuwezi kusema juu yetu. Tumekabiliwa na kubikiriwa, mauaji, udhia, cheko, uwongo, pamoja na kutimiwa vibaya kiroho hata na Mwili. Wengi wetu tumeteswa hivi. pia baadhi wetu wemekuwa ndio watesi wetu. Mungu ameacha Lango wazi kwa moyo safi unaotubu.Yeye ataka sisi tufanye vivyo hivyo. Ni vipi Pendo la Mungu laweza kung'aa, kama sio kupitia Msamaha na upendo wetu? Na ni vipi yule mtu mbaya anaweza kuokolewa.

Mwanadamu amezaliwa na asili ya dhambi. Tunapata kila aina ya wanaume na wanawake walio shushwa wakiwa na uweza wa uovu dhidi ya mwanadamu mwenzake, hi yategemea mazingira huyu alilelewa ndani na uweza wa tabia ya huyo mtu.

Mungu hukokota watu wamjie, lakini ametuachia jugumu la kuwa kielelezo cha upendo na Msamaha wake, jinsi Yesu alivyokuwa. Ni kupitia tu mifereji za rehema. Ni kwa sababu upendo mkubwa wa Mungu na Msamaha kwetu sisi alituma Mwanawake wa pekee kufa msalabani ilitokolewa. Hii ni gharama ya namna gani? (Yohana 3:16-17 Kwa maana jnsi hii Mungu aliupenda uliwengu, hata akamtoa Mwanawake pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. 17. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewa katika yeye.)

1. Samehe au Mungu hata Kusamehe.

Yesu, mwenyewe, aeleza haya katika hadithi anapo jibu Petro Mtume swali hili. “Ni mara ngapi nita msamehe ndugu yangu?”

Mathayo 18:21-35

21. Kisha Petro akamwendea akamwambia, **Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe?** Hata mara saba?

22. **Yesu akamwambia** Sikuambii mara saba, **hata saba mara sabini**.

23. Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme moja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake.

24. Alipoanza kuifanya aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi.

25. Naye alipo kosa cha kulipa,bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake,na vitu vyote alivyo navyo, ikalipe ile deni.

26. Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nita kulipa yote pia.

27. Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni.

28. Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia, akamkamata, akamshika koo, akisema, Nilipe uwiwacho.

29. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake akamsihi, akaisema, Nivumilie, nami ntikulipa yote pia.

30. Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni.

31. Basi wajoli wake walipo yaona yaliyotendeka, walisikitika sana wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka.

32. Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe ile deni yote, uliponisihi;

33. nawe je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?

34. Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hat atakapoilipa ile deni yote.

35. Ndivyo na Baba wangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake.

Mathayo 6:14-15

14. Kwa maana **mkiwasamehe** watu makasa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe nyinyi.

15. Bali **msipowasamehe** watu makosa yao, **wala Baba yenu hatawasamehe nyinyi makosa yenu.**

Kwa nini Mungu anatamani kuweka huru toka dhambini hukata kutusamehe dhambi ya kutosamehe? Kwa sababu Mungu ana haki kamilifu. Alitusamehe kabisa.Twahitaji kusamehe wengine kikamilifu.

Tunaweza kufananisha kutosamehe na mbegu ya gugu.Yamea kama haiwezi kung'olewa na kutupwa kando. Yaanza kufikiliza uharibifu ya mbegu njema maishani mwetu, ikiweka kizuizi kati yetu na Mungu. Ambaye hawezi kuishi na dhambi. Asema,

kwa hukumu tuhukumuyo nayo watu tutahukimiwa.Tunahitaji kutubu, samehe, kusafisha maisha yetu ya kutosamehe jinsi tunapo fanya kila dhambi iwayo anayotufunuliwa.

Hii ni ngumu kuikubali wakati mtu anapo tenda dhambi mbaya dhidi yako. Yasaidia kutambua kwamba watu huwacha waliyojifunza. Mtu anajua ukatili atazalisha ukatili. Yeye hawezi kupenda au kuwa mpole mpaka ajipe nafasi ya kujifunza na kupitia upendo. Mtu aliye tawalwa, baadaye atatawala na kutafuta kuongoza wengine, katika uweza wowote. Mtu aliyelelewa katika Uchawi ataendelea katika uweza huo mpaka mtu atakapo mwonyesha njia bora ndipo atakapo kuwa huru kutoka fumbato hiyo.

Iwapo tuaweza kutizama watu na wazo la nafsi kufikiwa itakuwa rahisi kuelewa ubaya wao. Ikiwa tuaweza kuona zaidi ya uchungu wetu, na tuone uchungu wao, itakuwa rahisi kueleweka hata kama matendo yao haya kubaliki.

Wakati mmoja nilipo uliza Bwana, asemehe kuteswa kwa watoto katika maeneo yetu, Jawabu lake lilikuwa, “Iwapo ungeona kwa nini watu waovu wapo jinsi walivyo, ungeweza kuchukia mtu wowote ila kuwahurumia na kuwaombea ili nafsi zao ziokoke. Iwapo ungeza kuhizi uchungu, mateso, utupu na hatia wana ona, ungeliweza kuwahurumia jinsi ninavyofanya badili ya kuwachukia kimwili. Chukia dhambi, na sio mtu.

Luka 6:37

37. **Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa**; msilaumu, nanyi hamtalaumiwa; **achilieni, nanyi mtaachiliwa**.

Luka 11:4

4. **Utusamehe** dhambi zetu, kwa kuwa sisi **nasi tunamsamehe** kila tumwiaye. Na usitutie majaribuni (lakini tuokoe na yule mwovu)

Luka 17:3-4

3. Jilindeni: kama ndugu yako akikosa, mwonye: akitubu msamehe.

4. Na **kama akikukosa** mara saba katika siku, **na kurudi kwako mara saba, akisema, Nemetubu, msamehe.**

Marko 11:25-26

25. Nanyi **kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu: ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na nanyi makosa yenu**.

26. Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.

Yamaanisha nini “mkiwa na neno juu au na mtu?” Ina maanisha kuwa na kila sababu ya kukasirika, kukwasa, au kuumiza kwa kulipiza yaliyo fanywa kwako. Tambua asema

lolote kumaanisha siso baadhi ya walio tukwasa, walakini wote.Yesu alituachia Mfano wa ajabu katika urejeo ya wale waliokuwa wakimsulubisha.

(Luka 23:33-34 Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulubisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume an mmoja upande wa kushoto. 34. **Yesu akasema, Baba, uwasemehe, kwa kuwa hawajui watendalo.....**

Mathayo 27:37-44

37. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaka yake, yaliyoandikwa, HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAUDI.

38. Wakati uo huo wanyang'anyi wawiliwakasulubiwa pamoja naye, mmoja mkono wa kuume na mmoja mkono wa kushoto.

39. Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa -tikisa vichwa vyao, wakisema.

40. Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi yako; ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, shuka msalabani.

41. Kadhalika na wale wakuu wa makuhani wakamdhihaki pamoja na waandishi wa wazee, wakisema Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe.

42.Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tuta mwamini.

43. Ametegemea Mungu, na mwokoe sasa, na kama anamtaka; kwa alisema Mimi ni mwana wa Mungu.

44. Pia wale wanyang'anyi walio sulubiswa pamoja naye walimshtumu vile vile.

Huu ni mfano gani wa ajabu wa msamaha!!!! Hata katika utungu wa kufa, moyo wake ulijawa na msamaha, na upendo, alio unena juu ya walio mdhihaki.

Warumi 5:8

8. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi**, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi.**

2. Samehe Jinsi Mungu Amekusamehe.

Wakolosai 3:12-13

12. Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendawao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema,unyenyekevu, upole, uvumilivu;

13. **Mchukuliana**, na **kusemeheana, na mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake: kama alivyowasamehe** nyinyi, vivyo na nanyi.

Yesu alitupa mfano jinsi ya kuomba. Msamaha ni wa maana aliyejumulisha katika mfano wa maombi yake.

Mathayo 6:9-13

9. Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje.

10. Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni .

11. Utupe riziki yetu.

12. Utusemehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.

13. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu, kwa kuwa ufalme niwako, na nguvu, na utukufu, hata milele.

Waefeso 4:32 **Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi,wenye huruma,mkisameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.**

3. Msamaha lazima utoke moyoni

Dhahiri hili huleta mashaka. Moyo uliumizwa toka kwa jiraha lilo kuja kwetu hauoni Pendo kuelekea mtu aliyetujeruhi.

Tuna pande mbili za hii hali:

> **1**.Pendo la moyo wetu ni pendo letu kwa Mungu. Je tuampenda Mungu kiasi cha kutoa wokovu kwa wanao tukosea? Katika kila hali lazima tuendelee sawa sawa jinsi Mungu ana tu ongoza ili tusijeweke katika hatari zaidi. Shauku lake ni kuokoa nafsi, sio kuiumiza wasio na hatia, au yule mkosaji, au aliyekosewa. Iwapo mkosaji atakata toleo la wokovu wa Mungu, Mungu ndiye hakimu wa nafsi zao, na sio sisi.Yeye atalipa maovu na haki yake. Hii si shughuli yetu. Shughuli yetu ni tusije tukawa jiwe la ukwaso katika nafsi zetu ndani ya wokovu, au kwa njia ya wakosaji kuingia wokovu, kwa kushikilia kutosamehe. Lazima twaachilie kutoka deni la dhambi dhidi yetu. Ni nafasi ya Mungu, sio yetu, kuendelea kuhesabu mambo ya nafsi ya mwanadamu.Yeye anaweza kuhukumu kwa haki. Itakuwa mwisho wenye huzuni kwetu, iwapo wakosaji au watesi wetu watatubu kwa kweli na kuenda mbinguni na tuenda katika Mateso ya milele kwa sababu tulikata kusamehe yeye.
>
> **2. Pendo huwa huruma kwa nafsi iliyo potea tu, na wakati tumejazwa na Roho wa Mungu, yeye ana wezesha sisi. Hatuwezi sisi, lakini na Mungu MAMBO YOTE, yawezakana. (Marko 9:23 Yesu akamwambia, Ukiweza ! Yote yawezakana kwake aaminiye.)**

Kuna hali mbaya sana wakati mwingine katika maisha. Ni Mungu peke yakee aweza kupitiliza katika hayo. Tukijaribu kung'ang'ana kujipiliza kwa uweza wetu tuta kuwa na uchungu, kutosamehe; na baadaye, kupoteza nafsi zetu.

Mathayo 18:32-35.

32. Ndipo **bwana** akamwita **akamwambia**, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi.

33. Nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako; kama mimi nilivyokurehemu wewe?

34. Bwana wake akaghadhika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote.

35. Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda, ninyi, misiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake.

6)UBATIZO WA TOBA (MAJI)

Yohana 3:5

5. **Yesu akajibu**, Amin, amin, nakuambia**, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.**

Marko 16:16

16. **Aaminiye na kubatizwa ataokoka**; asiyeamini,atahukumiwa.

Mchungaji Paulo Cross hueleza Ubatizo wa hivi “Ubatizo wa maji haufanyi mtu kuokoka, Lakini waonyesha wao washa okoka. Kwa hivyo ni upitilizo wa nje wa kuonyesha mabadiliko ya maishani mwetu. Yaonyesha kwamba Mauti au kufa kwa mtu wa kale, wanavyo zikwa ndani ya maji, na ufufuo wa mtu mpya wanapojitokeza kwa maji hayo. (Soma Warumi 6:2-4, Matendo ya mitume 10:47, Waefeso 2:1-10)

Ubatizo ni wa kila mmoja

1 Wakorintho 12:13 Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote **tulibatizwa** kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.

Ubatizo sio tu amri bali ni toleo la ajabu Bwana ametoa. Hutupa sisi **UBATIZO WA MAJI UWAKILISHAPO USAFISHO NA ONDOLEO LA DHAMBI ZETU.** Huondoa dhambi zetu jinsi Mashariki ilivyo mbali na Magharibi. Na, kuongezea, Mungu hutupa tunuko kuu, ambalo ni **UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU KUTUPA NGUVU ZA KUTUNZA UTAKATIFU ALIYE TUPA WAKATI ALIPO SAFISHA NA KUONDOA DHAMBI ZETU.**

Hili tendo la ubatizo halisafishi na kuonda dhambi zetu. Lakini Usafisho unafanywa ndani mwetu na Roho wa Mungu, Hi ni kufanya agano pamoja na Mungu, likishuhudiwa Naye, na muhudumu Wake, na wakati mwingine, hata kusanyiko lote. Lazima lifanywe katika utii na kweli Kwake.Yeye huitikia moyo ulio kweli kwa kusafisha na kuondoa dhambi zetu.

Mathayo 3:1-6

1. Siku zile aliondoka Yohana Mbatizaji akihubiri kaitka nyika ya Uyahudi, na kusema,

2. **Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.**

3. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake.

4. Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, mshipi wa ngozi kiunoni mwake. na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu.

5. **Ndipo walipomwendea** Yerusalemu, na Uyahudi wote, na Yordani;

6**. Naye akawabatiza kaitka mto wa Yordani; huku wakiziungama dhambi zao.**

Matendo ya Mitume 10:48

48. Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha.

Matendo ya Mitume 22:16

16. Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukilitilia jina lake.

Ni ya muhumu sana kutambua ya kwamba walio enda katika ibada za Ubatizo waYohana **wali kiri dhambi zao na kilitia jina la Mungu**. Hi haikuwa kukiri mbele ya mwanadamu..... bali walitia jina la Mungu.Yeye ndiye Msamaha, msamaha wake uta wosha na kuonda dhambi ya kale na kutufanya Viumbe vipya. Hamna Mwanadamu anaweza kusamehe dhambi zetu, au hamna mtu aliye na uweza wakujitoa na kupokea dhabihu zetu kwa ajili ya kusamehe dhambi zetu. (Waebrania 10:11-13) Hii ni haki ya Bwana Yesu. Yeye alilipa gharama yakukuwa kwetu kuhani Mukuu alipo kufa kwa ajili yetu Msalabani, Akifanyika kweli dhabihu yetu kamilifu. Ni yeye anayefanya sisi kuwa kiumbe kipya cha utakatifu wake ulio safi.

Waebrania 10:11-12

11. Na kila kuhani husimama kila siku akifanya ibada, na kutoa dhabihu zile zile mara nyingi: ambazo haziwezi kabisa kuondoa dhambi.

12. Lakini **huyu alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu**.

Waebrania 7: 25-27

25. Naye, **kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye**; maana **yu hai siku zote ili awaombee.**

26. Maana ilitupasa sisi kuwa na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu, asiyekuwa na uovu, asiyekuwa na waa lo lote, aliyekuwa kuliko mbingu.

27. **ambaye hana haja kila siku**, mfano wa wale makuhani wakuu wengine**, kwanza kutoa dhabihu** kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; **maana yeye alifanya hivi mara moja, alipojitoa nafsi yake**.

Jambo lingine la kustaajabisha kuhusu Ubatizo wa Yohana, ni kwamba alibatiza ndani ya mto ili mwili wote ungezamishwa. Hawa watu walitubu dhambi ZAO ZOTE na waka safishwa KIKAMILIFU SAFI, NA KUSAMEHEWA NA MUNGU. Huo mto uliwakilisha ukamilifu walipo zamishwa. Hi iliwafunika kote. Ikawa vile Bwana afunga Mikono yake mitakatifu kuwazongomeza wao anavyowasafisha dhambi zao.

Pia tuliambiwa kubatizwa katika jina la Yesu. Kwa nini? Kwa sababu ni Yesu Kristo aliye lipa gharama ya msamaha wetu. Hii ni dhabihu ya thamana kwetu sisi tunayo itambua toka kwake. Twaambia walimwengu twaamini Yeye na kubali kipawa chake, Msamaha wake. Hapo twakubali kwamba tume tenda dhambi na tuna mhitaji Yeye.

Kwa Ondoleo La Dhambi:

Marko 1:4-5

4.Yohana alitokea, akibatiza nyikani na kuhubiri **ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi** .

5. Wakamwendea, nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, **wakabatizwa wote katika** mto wa Yordini, wakiziungama dhambi zao.

8. **Mimi nilibatiza kwa maji**; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu.

Matendo ya Mitume 22:16

16. Basi sasa, unakawilia nini? **Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukilitilia jina lake.**

Ona hapa pia kukiri.Kwamba kukiri na kubatizwa huenda pamoja.

Marko 16:15-16

15. Akawambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.

16. **Aaminiye na kubatizwa ataokoka**; asiyeamini, atahukumiwa

Maelekezi Dhairi ya Ubatizo

Kunayo namna dhairi ya kubatiza.Wanafunzi waliambiwa enendeni basi mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, Mkawabatize kwa Jina la Baba , na Mwana na Roho Mtakatifu. (Mathayo 28:19) Tuna batiza kwa kuzamisha Maana Yesu, aliye kuja kama kielelezo kwetu alibatizwa na Yohana Mbatizaji namna hii.

7) UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NA MOTO

Ule ubatizo Yesu alileta: Ubatizo wa Roho mtakatifu na Moto.

Yesu alipokuwa anazungumza na Nikodemo katika kitabu cha Yohana sura ya tatu. Ali dhirisha kwamba tunahitaji Ubatizo wa aina mbili wote; wa Maji na wa Roho. Asema iwapo hatupokee Roho hatuwezi kuingia katika ufalme wa Mungu.Yesu, alipokea ubatizo wa aina mbili yote.

Mathayo 3:16-17

16. Mara tu Yesu alipokwisha batizwa, alitoka majini; ***na*** ghafla mbingu zikafunguka, akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kutua juu yake.

17 Sauti kutoka mbinguni ikasema, (“Huyu ndiye Mwanangu mpendwa, nimependezwa naye.”)

Alipo pokea Ubatizo wa Roho, hapo Roho alimtuma na kumwongoza kuenda nyikani kabiliana na kujaribiwa na Ibilisi basi.

Iwapo YESU alihitaji Roho pia nasi tunahitaji.

Yohana alihaidi ya kwamba Yesu atabatiza sisi kwa Roho mtakatifu na Moto.

Yesu, asema atatuma Roho. Hakika atueleza ilimpasa afe na aondoke duniani ili atuletee Roho (Yohana 16:7 Lakini mimi **nawaambia kweli, niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu**.) Roho Mtakatifu kipawa kwetu. (Matendo ya mitume 2:38 Petro akawaambia, Tubuni **mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nayi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.)**

Yohana 3:5 -6

5 Yesu akamjibu, Kweli nakwambia, **mtu asipozaliwa kwa maji *na* Roho, hawezi kamwe kuingia katika ufalme wa Mungu**.

6 **Mtu huzaliwa kimwili kwa baba na mama, lakini huzaliwa kiroho kwa Roho**.

Mathayo 3:11-17

11. Mimi ninawabatizeni kwa maji kuonyesha kwamba mmetubu**. Lakini yule anayekuja baada yangu ana uwezo kuliko mimi. Mimi sistahili hata kubeba viatu vyake. Yeye atawabatizeni kwa Roho Mtakatifu na kwa moto**.

12. Yeye anashika mkononi chombo cha kupuria nafaka, ili aipure nafaka yake; akusanye ngano ghalani, na makapi ayachome kwa moto usiozimika.

13. **Wakati huo Yesu alitoka** Galilaya akafika katika mto Yordani, akamwendea Yohane **ili abatizwe naye**.

14. Lakini Yohane alijaribu kumzuia akisema, “Je, wewe unakuja kwangu? Mimi hasa ndiye ninayehitaji kubatizwa nawe.”

15. Lakini Yesu akamjibu, “Acha tu iwe hivyo kwa sasa, maana kwa namna hii inafaa tuyatekeleze yale yote Mungu anayotaka.” Hapo Yohane akakubali.

16. Mara tu Yesu alipokwisha batizwa, alitoka majini; na ghafla mbingu zikafunguka, akaona Roho wa Mungu akishuka kama njiwa na kutua juu yake.

17. Sauti kutoka mbinguni ikasema, “Huyu ndiye Mwanangu mpendwa, nimependezwa naye.”

Mathayo 4:1

1. Kisha **Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi.**

Roho Mtakatifu hufanya makao ndani mwetu wakati tunapo pokea wokovu. Huanza kutufundisha, kutuongoza na kadhalika. Lakini, kuna wakati maalumu anapo kuja tena. Anaweza kwa ghafula, au aje wakati fulani baadaye tunapokuwa tayari. Huu ndiwo wakati Roho Mtakatifu hutupa nguvu na mamlaka, wakati tunapojitoa mhanga kwake. Mpaka wakati wanafunzi walipo jazwa Roho Mtakatifu ndipo walikuwa na Ushuja, ujasiri na ujuzi wa kusimama mbele za umati uliokuwa tayari kuwatesa.

Kubatizwa katika Roho ni wakati wa ufanuo wa kiroho ambako Roho Mtakatifu huleta ukweli wa Mungu kwetu katika hali ya ukamillifu ambako tunakuwa wajisiri na kujazwa na uweza wake na miujiza unao sababisha kushudiwa kwake. Tuna ingia katika utendaji wa maisha yetu ya Kikristo katika kuelekea kupya kama walio tengwa kwa upako wa Kristo. Hatunywi tena bali tunaanza kumimina kwa wengine yale Mungu alimimina kwetu.

Yohana14:15-17

15. Mkinipenda mtazishika amri zangu.

16. Nami **nitamwomba Baba naye atawapeni Msaidizi mwingine**, atakayekaa nanyi milele.

17. Eye ni **Roho wa kweli. Ulimwengu hauwezi kumpokea** kwa sababu hauwezi kumwona wala kumjua. **Lakini ninyi mnamjua kwa sababu anabaki nanyi na yu ndani yenu.**

Waefeso 5:18

18. Acheni kulewa divai maana hiyo itawaangamiza, **bali mjazwe Roho Mtakatifu**

Mathayo 20:22-23

22. **Yesu akajibu akasema hamjui** mnaloliomba. Je! Mweweza kunywa kunywea kikombe nitakachonywea mimi? Wakamwambia, Twaweza.

23. Akawaambia, **Hakika mtakinywea kikombe changu; lakini kuketi mkono wangu wa kuume na mkono wangu wa kushoto, sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekewa tayari na Baba yangu.**

Mara nyingi katika jamii, watu kwa urahisi hawaja sikia ya kwamba kuna toleo maalumu la Mungu, ambalo ni Roho Mtakatifu, amabaye ni wa kuwezeza sisi kuishi katika utakatifu.Kuna mfano wa Jambo hili laelezwa katika Biblia. Tambua kwamba Paulo ananena na wanafunzi..... watu wa Mungu ambao hawakuwa na ufahamu sana.

Matendo ya mitume 19:1-6

1.Wakati Apolo alipokuwa Korintho, Paulo alisafiri sehemu za bara, akafika Efeso ambako aliwakuta wanafunzi kadhaa.

2**. Akauliza**, “Je, **mlipopata kuwa waumini mlipokea Roho Mtakatifu**?" Nao wakamjibu, La! Hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatujasikia.”

3. Naye akasema, “Sasa mlipata ubatizo wa namna gani?” Wakamjibu, “Ubatizo wa Yohane.”

4. **Naye Paulo akasema, “Ubatizo wa Yohane ulikuwa wa kuonyesha kwamba watu wametubu. Yohane aliwaambia watu wamwamini yule ambaye alikuwa anakuja baada yake, yaani Yesu.”**

5. **Baada ya kusikia hayo, walibatizwa kwa jina la Bwana Yesu**.

6. **Basi, Paulo akawawekea mikono, na Roho Mtakatifu akawashukia, W**akaanza kusema lugha mbalimbali na kutangaza ujumbe wa Mungu.

Maombi yafutayo ni mfano Jinsi ya kuomba kupokea hali yako kuzaliwa mara ya pili. Mungu husikia maombi ya kweli. Daudi aliomba Zaburi 51:10 Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho ilitulia ndani yangu.

Tanaambua kwamba unapo omba, amini kwamba utapata Uwepo wake maishani mwako. Iwapo una tatizo katika kuamini uliza Msaada wake. Tuna ona katika Marko 9:24 Hadithi ya mtu aliye mjia Yesu kwa ajili ya uponyaji wa mwana wake. Neno la tuambia, mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutoamini kwangu. Na kijana akaponywa. Mungu aanatamni kusaidia wewe.

Tunaambiwa tu ombe, katika Jina la Yesu na kuelekea Baba aliye mbinguni: Katika 6:9 baada ya haya Ombeni hivi, Baba aliye mbinguni, jina litukuzwe. na Yohana 16:26 Siku hiyo mta omba katika jina langu.

Waweza kutimia Ombi lifuatalo kusadia kutafuta Mungu na hali ake ya kuzaliwa upya.

MFANO WA MAOMBI

Baba yetu wa mbinguni, Naja kwako katika jina la Yesu.

Na omba kwamba unisamehe dhambi zanngu na usafisha mawaa yake toka maishani mwangu.

Nisaidie kusamehe walio nitenda dhambi na walio nikosea.

Bwana nakiri ya kwamba nimekokosea na nimekutenda dhambi .

Nisadie niwe hodari wa kutotenda dhambi katika maeneo haya.

Na omba hekima, maarifa, na ufahamu wa njia zako.

Ninapo anza kuomba na kutafuta na kusoma kuhusu wewe katika Neno lako.

Na omba uje maishani mwangu na unijaze na Roho wako .

Bwana, nina kushukuru kwa kuni vuta, kwa wakati huu wa kujifunza kutoka kwako.

Nina kushsukuru wewe Yesu, kwa kuja kuniokoa, kwa kuandaa njia kwa ajili yangu, kuja kuishi katika ufalme wako mwisho mwa maisha haya.

Nina kushukuru kwa kuugusa, mwili, nafsi, na roho kwa uponyaji wako,

Nina kushukuru kwa kunitia moyo, kwa ajili ya nguvu za kukabili majiribu na kuyashinda.

Na omba ya kwamba utasababisha dhamira yangu kutenda wema siku zote ,kwamba utafanya kinachohitachika kushika uangalifu na kulenga kwangu kuwe ni kwako.

Nina omba katika jina la thamana la Yesu.

AMINA.

MAISHA YETU MAPYA.

Tupo wapi katika hatua hii? Tume amini, tume kiri, tume tubu, na kusiacha dhambi zetu, tume samehewa, tumesamehe wenzetu, tumebatizwa,na kutafuata Roho Mtakatifu na ujazo wake maishani mwetu.

Zifuatazo ni Mistari za Bibilia za kukusadia katika matembezi yako mapya. Unaingia katika kutunukishwa na kuitimiliza Safari. Usi tumie sehemu hii kama amri za uhalalisho. Bali tumia sehemu kama maelekezi ya kujua kile Mungu anakutakia na ufuate. Fanya vitu vyote kana kwamba Mungu yupo nawe hapo ulipo. Yeye yupo. Anatamani ushirika wako, na uhusiano wako. Tengeneza maisha yako mapya na yeye kuwa mshirika nawe, maana u sehemu mpya ya Bi arusi aliye ozwa kwake Yesu. Yeye anakupenda. Kila maelekezi atoayo yanafaa kwako, maana mawazo yake kwako ni njema na sio ovu.

Sisi ni akina nani katika Kristo

Tulipo mpokea Kristo na tuka batizwa katitka maisha mapya tulisafishwa tukawa Safi, tukafanywa upya, na hakuna hatia ya dhambi zilizo nyuma yetu. Lakini tu watoto katika Kristo. Lazima tukuwe na tukomae. Watu wengine watarajia waKristo wapya kukoma hapo na hapo. Hii haifanya kazi hivyo lazima tujifunze mfano wa Kristo jinsi ya kutembea na kukimbia. Na watu wana viwango vya kukuwa tofauti. Watu wana nguvu na udhaifu tofauti maishani mwao ambako Mungu anakabiliana nao. Hii ina gharimu kujitoa kwake Mungu. Kila mtu anaweza kujikwaa na hata wakati mwingine kuanguka lakini mpaka aamke na kuanza tena. Sehemu iliyo bora kwa yote ni kwamba, tunapojikwaa, tunaye wakili na Baba, Yesu Kristo aliye mwenye haki, atafutaye kuturejesha na kutushikilia kwa njia iliyo kweli. Yeye hataki kutupoteza.Tusijiruhusu kukaa katika hali ya kushindwa au kuanguka, ni lazimu tutambue tume anguka, tunahitaji kutubu, na kuamka, na kuendelea na yeye ndilo shauku lake.

1 Yohana2:1

1.Watoto wangu wadogo, ninawaandikieni mambo haya, kusudi msitende dhambi. **Lakini, ikijatokea mtu akatenda dhambi, tunaye mmoja ambaye hutuombea kwa Baba, ndiye Yesu Kristo aliye mwadilifu kabisa.**

2 Wakorintho 5:17-20

17. **Mtu yeyote akiungana na Kristo huwa kiumbe kipya,** mambo ya kale yamepita, hali mpya imefika.

18. Yote ni kazi ya **Mungu** mwenye **kutupatanisha sisi naye kwa njia ya Kristo, akatupa nasi jukumu la kuwapatanisha watu naye.**

19. Ndiyo kusema: Mungu, amekuwa akiupatanisha ulimwengu naye kwa njia ya Kristo, bila kutia maanani dhambi zao binadamu. Yeye ametupa ujumbe kuhusu kuwapatanisha watu naye.

20. Basi, sisi tunamwakilisha Kristo, naye Mungu mwenyewe anatutumia sisi kuwasihi ninyi. Tunawaombeni kwa **niaba ya** Kristo, mpatanishwe na Mungu.

Wagalatia 6:15

15. **Kutahiriwa au kutotahiriwa si kitu; cha maana ni kuwa kiumbe kipya.**

Waefeso 2:4-8

4. Lakini **Mungu** ni mwenye huruma nyingi. **Alitupenda kwa mapendo yasiyopimika,**

5. **hata, ingawa tulikuwa tumekufa kwa sababu ya dhambi, alitufanya hai pamoja na Kristo. Kwa neema ya Mungu ninyi mmeokolewa.**

6. Kwa **kuungana na Kristo Yesu, Mungu alitufufua pamoja naye, tukatawale pamoja naye mbinguni.**

7. **Ndivyo alivyopenda kuonyesha kwa watu wa nyakati za baadaye, ukuu wa neema yake aliyotujalia kwa ukarimu katika kuungana kwetu na Kristo Yesu.**

8. Maana, kwa neema ya Mungu mmekombolewa kwa njia ya imani. Jambo hili si matokeo ya juhudi zenu, **bali ni zawadi ya Mungu**

Warumi 8:1

1. Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu kwa wale ambao katika maisha yao wameungana na **Kristo.**

Warumi 8:34

34. Ni nani atakayewahukumu? Hakuna! Maana **Kristo** ndiye **aliyekufa**, tena **alifufuka kutoka wafu na anakaa upande wa kulia wa Mungu. Yeye anatuombea!**

2 Wakorintho 3:18

18. Basi, **sisi sote** ambao nyuso zetu hazikufunikwa, twaonyesha kama katika kioo, utukufu wa Bwana; **tunabadilishwa tufanane zaidi na huo mfano wake kwa utukufu mwingi zaidi. Hiyo ni kazi yake Roho wa Bwana.**

Wafilipi 3:21

21. **Atakayeubadili mwiliwetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu,** kwa uweza ule mbao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake.

1 Yohana 3:2

2.Wapenzi wangu, sisi ni watoto wa Mungu sasa, lakini bado haijaonekana wazi jinsi tutakavyokuwa. **Lakini tunajua** kwamba wakati Kristo atakapotokea, tutafanana naye kwani tutamwona vile alivyo.

Ni kitu gani tunacho amini?

Matendo ya mitume 17:24-31

24. Mungu, aliyeumba ulimwengu na vyote vilivyomo, ni Bwana wa mbingu na nchi; yeye hakai katika hekalu zilizojengwa na watu.

25. Wala hatumikiwi kwa mikono ya watu kana kwamba anahitaji chochote kile, kwa maana yeye mwenyewe ndiye anayewapa watu uhai, anawawezesha kupumua na anawapa kila kitu.

26 .Kutokana na mtu mmoja aliumba mataifa yote na kuyawezesha kuishi duniani kote. Aliamua na kupanga kabla kabisa lini na wapi mataifa hayo yangeishi.

27. Alifanya hivyo, ili mataifa hayo yapate kumfuata, na kama vile kwa kupapasapapasa, yapate kumfikia. Hata hivyo lakini, Mungu hayuko mbali na kila mmoja wetu.

28. Kama alivyosema mtu mmoja: (dani yake yeye sisi tunaishi, tunajimudu, na tuko!) Ni kama washairi wenu wengine walivyosema: (si ni watoto wake.)

29. Ikiwa basi, sisi ni watoto wa Mungu, haifai kumfikiria Mungu kuwa kama dhahabu, fedha au hata jiwe lililochongwa na kutiwa nakshi na binadamu.

30. Mungu alifanya kama kwamba haoni nyakati zile watu walipokuwa wajinga. Lakini sasa, anaamuru watu wote kila mahali watubu.

31. Kwa maana amekwisha weka siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki kwa njia ya mtu mmoja aliyemteua. Mungu amewathibitishia wote jambo hili kwa kumfufua mtu huyo kutoka wafu!

Maelekezi ya Yesu kuhusu Maisha ya Kikristo

Mathayo 5:1-48

1.Yesu alipoyaona makundi ya watu, alipanda mlimani, akaketi. Wanafunzi wake wakamwendea,

2. naye akaanza kuwafundisha:

3. “Heri walio maskini rohoni, maana ufalme wa mbinguni ni wao.

4. Heri walio na huzuni, maana watafarijiwa.

5. Heri walio wapole, maana watairithi nchi.

6. Heri wenye njaa na kiu ya kufanya atakavyo Mungu, maana watashibishwa.

7. Heri walio na huruma, maana watahurumiwa.

8. Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu.

9. Heri wenye kuleta amani, maana wataitwa watoto wa Mungu.

10. Heri wanaoteswa kwa sababu ya kufanya atakavyo Mungu, maana ufalme wa mbinguni ni wao.

11. “Heri yenu ninyi watu wakiwatukana, wakiwadhulumu na kuwasingizia kila aina ya uovu kwa ajili yangu.

12. Furahini na kushangilia maana tuzo lenu ni kubwa mbinguni. Hivyo ndivyo walivyowadhulumu manabii waliokuwako kabla yenu.

13. “Ninyi ni chumvi ya dunia! Lakini chumvi ikipoteza ladha yake itakolezwa na nini? Haifai kitu tena, ila hutupwa nje na kukanyagwa na watu.

14. “Ninyi ni mwanga wa ulimwengu! Mji uliojengwa juu ya mlima hauwezi kufichika.

15. Wala watu hawawashi taa na kuifunika kwa chungu, ila huiweka juu ya kinara ili iwaangazie wote waliomo nyumbani.

16. Vivyo hivyo, ni lazima mwanga wenu uangaze mbele ya watu, ili wayaone matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.” Kuhusu Sheria

17. “Msidhani ya kuwa nimekuja kutangua Sheria ya Mose na mafundisho ya manabii. Sikuja kutangua bali kukamilisha.

18. Kweli nawaambieni, mpaka hapo mbingu na dunia zitakapopita, hakuna hata nukta moja au sehemu ndogo kabisa ya Sheria itakayoondolewa, mpaka yote yametimia.

19. Basi, yeyote atakayevunja hata amri moja ndogo kuliko zote, na kuwafundisha wengine wafanye hivyo, huyo atakuwa mdogo kabisa katika Ufalme wa mbiguni. Lakini yule atakayezishika na kuwafundisha wengine, huyo atakuwa mkubwa katika Ufalme wa mbinguni.

20. Ndiyo maana nawaambieni, wema wenu usipozidi ule wa Mafarisayo na walimu wa Sheria, hamtaingia kamwe katika Ufalme wa mbinguni.

21."Mmekwisha sikia ya kuwa watu wa kale waliambiwa: (siue! Atakayeua lazima ahukumiwe)

22. Lakini mimi nawaambieni, yeyote anayemkasirikia ndugu yake, lazima ahukumiwe. Anayemdharau ndugu yake atapelekwa mahakamani. Anayemwita ndugu yake: Pumbavu atastahili kuingia katika moto wa Jehanamu.

23. Basi, ukipeleka sadaka yako mbele ya madhabahu na hapo ukakumbuka kwamba ndugu yako ana ugomvi nawe,

24. iache sadaka yako mbele ya madhabahu, nenda kwanza ukapatane na ndugu yako, ndipo urudi ukatoe sadaka yako.

25. “Patana na mshtaki wako upesi mkiwa bado njiani, kwenda mahakamani. La sivyo, mshtaki wako atakukabidhi kwa hakimu, naye hakimu atakukabidhi kwa askari, nawe utafungwa gerezani.

26. Kweli nakwambia, hutatoka humo mpaka umemaliza kulipa senti ya mwisho. Kuhusu uzinzi

27. “Mmesikia ya kuwa watu waliambiwa: (usizini!)

28. Lakini mimi nawaambieni, atakayemtazama mwanamke kwa kumtamani, amekwisha zini naye moyoni mwake.

29. Basi, kama jicho lako la kulia linakukosesha, ling'oe ukalitupe mbali. Afadhali zaidi kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako, kuliko mwili wako wote kutupwa katika moto wa Jehanamu.

30. Na kama mkono wako wa kulia unakukosesha, ukate ukautupe mbali. Afadhali zaidi kupoteza kiungo kimoja cha mwili, kuliko mwili wako wote uende katika moto wa Jehanamu.

31. “Ilikwisha semwa pia: Anayemwacha mke wake, yampasa ampe hati ya talaka.

32. Lakini mimi nawaambieni, anayempa mkewe talaka, isipokuwa kwa sababu ya uzinzi, anamfanya azini; na mtu akimwoa mwanamke aliyepewa talaka, anazini. Kuhusu kiapo

33. “Tena mmesikia kuwa watu wa kale waliambiwa: Usivunje kiapo chako, bali ni lazima utimize kiapo chako kwa Bwana. 34 Lakini mimi nawaambieni, msiape kamwe; wala kwa mbingu, maana ni kiti cha enzi cha Mungu;

35. wala kwa dunia, maana ni kiti chake cha kuwekea miguu; wala kwa Yerusalemu, maana ni mji wa Mfalme mkuu.

36. Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kuufanya hata unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.

37. Ukisema, Ndiyo, basi iwe Ndiyo; ukisema Siyo, basi iwe kweli Siyo. Chochote kinachozidi hayo hutoka kwa yule Mwovu.

38. “Mmesikia kwamba ilisemwa: Jicho kwa jicho, jino kwa jino.

39. Lakini mimi nawaambieni, usimlipize kisasi mtu mbaya. Mtu akikupiga kofi shavu la kulia, mgeuzie pia shavu la pili.

40. Mtu akikupeleka mahakamani kutaka kukuchukulia shati lako, mwache achukue pia koti lako.

41 Mtu akikulazimisha kubeba mzigo wake kilomita moja, ubebe kilomita mbili.

42. Akuombaye mpe, na mtu akitaka kukukopa kitu usimnyime.

43. “Mmesikia kwamba ilisemwa: Mpende jirani yako na kumchukia adui yako.

44. Lakini mimi nawaambieni, wapendeni adui zenu na kuwaombea wale wanaowadhulumu ninyi

45. ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana yeye huwaangazia jua lake watu wabaya na wema, na kuwanyeshea mvua watu wanyofu na waovu.

46. Je, mtapata tuzo gani kwa kuwapenda tu wale wanaowapenda ninyi? Hakuna! Kwa maana hata watoza ushuru hufanya hivyo!

47. Kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mmefanya kitu kisicho cha kawaida? Hata watu wasiomjua Mungu nao hufanya vivyo hivyo.

48. Basi, muwe wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.

Mathayo 6:1-34

1. “Jihadharini msije mkafanya matendo yenu mema mbele ya watu kusudi mwonekane nao. La sivyo, Baba yenu aliye mbinguni hatawapeni tuzo.

2. “Basi, unapomsaidia maskini, usijitangaze. Usifanye kama wanafiki wafanyavyo katika masunagogi na njiani ili watu wawasifu. Kweli nawaambieni, hao wamekwisha pata tuzo lao.

3. Lakini wewe unapomsaidia maskini, fanya hivyo kwamba hata rafiki yako asijue ufanyalo.

4. Toa msaada wako kwa siri, na Baba yako aonaye yaliyofichika, atakutuza.

5. “Mnaposali, msifanye kama wanafiki. Wao hupenda kusimama na kusali katika masunagogi na katika pembe za njia ili watu wawaone. Kweli nawaambieni, hao wamekwisha pata tuzo lao.

6. Lakini wewe unaposali, ingia chumbani mwako, funga mlango, kisha umwombe Baba yako asiyeonekana. Naye Baba yako aonaye yaliyofichika, atakutuza.

7. “Mnaposali, msipayuke maneno kama watu wasiomjua Mungu. Wao hudhani kwamba Mungu atawasikiliza ati kwa sababu ya maneno mengi.

8. Msiwe kama wao. Baba yenu anajua mnayoyahitaji hata kabla ya kumwomba.

9. Basi, hivi ndivyo mnavyopaswa kusali: Baba yetu uliye mbinguni: Jina lako litukuzwe.

10. Ufalme wako ufike. Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni.

11. Utupe leo chakula chetu tunachohitaji.

12. Utusamehe makosa yetu, kama nasi tunavyowasamehe waliotukosea.

13. Usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu.Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

14. “Maana mkiwasamehe watu makosa yao, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia.

15. Lakini msipowasamehe watu makosa yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu. Kuhusu kufunga

16. “Mnapofunga, msiwe na huzuni kama wanafiki. Wao hukunja nyuso zao wapate kuonekana na watu kuwa wanafunga. Nawaambieni hakika, hao wamekwisha pata tuzo lao.

17. Wewe lakini unapofunga, paka kichwa chako mafuta, nawa uso wako,

18. ili mtu yeyote asijue kwamba unafunga, ila ujulikane tu kwa Baba yako asiyeonekana. Naye Baba yako aonaye yaliyofichika atakutuza.

19. “Msijiwekee hazina hapa duniani ambako nondo na kutu huharibu, na wezi huingia na kuiba.

20. Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba.

21. Maana pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.

22. “Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho lako ni zima, mwili wako wote utakuwa katika mwanga.

23. Lakini ikiwa jicho lako ni bovu, mwili wako wote utakuwa katika giza. Basi, ikiwa mwanga ulioko ndani yako ni giza, basi, hilo ni giza la kutisha mno

24. “Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili. Maana atamchukia mmoja na kumpenda huyo wa pili; au ataambatana na mmoja na kumdharau huyo mwingine. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali pamoja.

25. “Ndiyo maana nawaambieni, msiwe na wasiwasi juu ya chakula na kinywaji mnavyohitaji ili kuishi, wala juu ya mavazi mnayohitaji kwa ajili ya miili yenu. Je, maisha ni chakula tu au zaidi? Na mwili, je, si zaidi ya mavazi?

26. Waangalieni ndege wa mwituni: hawapandi, hawavuni, wala hawana ghala yoyoye. Hata hivyo, Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, ninyi si wa thamani kuliko hao?

27. Ni nani miongoni mwenu kwa kuwa na wasiwasi sana anaweza kuuongeza muda wa maisha yake?

28. “Na kuhusu mavazi, ya nini kuwa na wasiwasi? Tazameni maua ya porini jinsi yanavyostawi. Hayafanyi kazi wala hayasokoti.

29. Lakini nawaambieni, hata Solomoni mwenyewe na fahari zake zote hakupata kuvikwa vizuri kama ua mojawapo.

30. Ikiwa basi Mungu hulivika hivyo jani la shambani ambalo leo liko na kesho latupwa motoni, je, hatafanya zaidi kwenu ninyi? Enyi watu wenye imani haba!

31. “Basi, msiwe na wasiwasi: Tutakula nini, tutakunywa nini, tutavaa nini!

32. Maana hayo yote yanahangaikiwa na watu wasiomjua Mungu. Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnahitaji vitu hivyo vyote.

33. Bali, zingatieni kwanza Ufalme wa Mungu na matakwa yake, na hayo mengine yote mtapewa kwa ziada.

34. Basi, msiwe na wasiwasi juu ya kesho; kesho inayo yake. Matatizo ya siku moja yanawatosheni kwa siku hiyo.

Mathayo 7:1-29

1. “Msiwahukumu wengine, msije nanyi mkahukumiwa na Mungu;

2. kwa maana jinsi mnavyowahukumu wengine, ndivyo nanyi mtakavyohukumiwa; na kipimo kilekile mnachotumia kwa wengine ndicho Mungu atakachotumia kwenu.

3. Kwa nini wakiona kibanzi kilicho jichoni mwa ndugu yako, na papo hapo huioni boriti iliyoko jichoni mwako?

4. Au, wawezaje kumwambia ndugu yako, Ndugu, ngoja nikuondoe kibanzi jichoni mwako, wakati wewe mwenyewe unayo boriti jichoni mwako?

5. Mnafiki wewe! Ondoa kwanza boriti iliyoko jichoni mwako na hapo ndipo utaona waziwazi kiasi cha kuweza kuondoa kibanzi kilichoko jichoni mwa ndugu yako.

6. “Msiwape mbwa vitu vitakatifu wasije wakageuka na kuwararua ninyi; wala msiwatupie nguruwe lulu zenu wasije wakazikanyaga.

7. “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, nanyi mtafunguliwa.

8. Maana, aombaye hupewa, atafutaye hupata, na abishaye hufunguliwa.

9. Je, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake akimwomba mkate, atampa jiwe?

10. Au je, akimwomba samaki, atampa nyoka?

11. Kama basi ninyi, ingawa ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri, hakika Baba yenu wa mbinguni atafanya zaidi: atawapa mema wale wanaomwomba.

12. “Watendeeni wengine yale mnayotaka wao wawatendee ninyi. Hii ndiyo maana ya Sheria ya Mose na mafundisho ya manabii.

13. “Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba. Kwa maana njia inayoongoza kwenye maangamizi ni pana, na mlango wa kuingilia humo ni mpana; waendao njia hiyo ni wengi.

14. Lakini njia inayoongoza kwenye uzima ni nyembamba, na mlango wa kuingilia humo ni mwembamba; ni watu wachache tu wanaoweza kuigundua njia hiyo.

15. “Jihadharini na manabii wa uongo. Wao huja kwenu wakionekana kama kondoo kwa nje, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali.

16. Mtawatambua kwa matendo yao. Je, watu huchuma zabibu katika miti ya miiba, au tini katika mbigili? La!

17. Basi, mti mwema huzaa matunda mema, na mti mbaya huzaa matunda mabaya.

18. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mema.

19. Kila mti usiozaa matunda mema utakatwa na kutupwa motoni.

20. Kwa hiyo, mtawatambua kwa matendo yao.

21. “Si kila aniambiaye, Bwana, Bwana, ataingia katika Ufalme wa mbinguni; ila ni yule tu anayetimiza mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.

22. Wengi wataniambia Siku ile ya hukumu: Bwana, Bwana! kwa jina lako tulitangaza ujumbe wako, na kwa jina lako tuliwatoa pepo na kufanya miujiza mingi.

23. Hapo nitawaambia: Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni mbele yangu, enyi watenda maovu.

24. “Kwa sababu hiyo, kila mtu anayeyasikia maneno yangu na kuyazingatia, anafanana na mtu mwenye busara, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba.

25. Mvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo. Lakini haikuanguka kwa sababu ilikuwa imejengwa juu ya mwamba.

26. “Lakini yeyote anayesikia maneno yangu haya bila kuyazingatia, anafanana na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga.

27. Mvua ikanyesha, mito ikafurika, pepo kali zikavuma na kuipiga nyumba hiyo, nayo ikaanguka; tena kwa kishindo kikubwa." Mamlaka ya Yesu

28. Yesu alipomaliza kusema maneno hayo, umati wa watu ukashangazwa na mafundisho yake. 29. Hakuwa kama walimu wao wa Sheria

AMRI MBILI KUU ZA YESU

Mathayo 22:36-36

36. “Mwalimu, ni amri ipi iliyo kuu katika Sheria ya Mose?”

37. Yesu akamjibu, “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa akili yako yote.

38. Hii ndiyo amri kuu ya kwanza.

39. Ya pili inafanana na hiyo: Mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe.

40. Sheria yote ya Mose na mafundisho ya manabii vinategemea amri hizi mbili.”

KATIKA TAMATISHO

Mathayo 25:31-46

31. “Wakati Mwana wa Mtu atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote wakiwa pamoja naye, hapo ataketi juu ya kiti chake cha enzi kitukufu,

32. na mataifa yote yatakusanyika mbele yake, naye atawatenganisha watu kama mchungaji anavyotenganisha kondoo na mbuzi.

33. Atawaweka kondoo upande wake wa kulia na mbuzi upande wake wa kushoto.

34. “Kisha Mfalme atawaambia wale walio upande wake wa kulia, `Njoni enyi mliobarikiwa na Baba yangu; pokeeni Ufalme mliotayarishiwa tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

35. Maana nilikuwa na njaa nanyi mkanipa chakula; nilikuwa na kiu nanyi mkanipa maji; nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha

36. nilikuwa uchi, mkanivika; nilikuwa mgonjwa nanyi mkaja kunitazama; nilikuwa gerezani nanyi mkaja kunitembelea.

37. Hapo, hao watu wema watamjibu mfalme Bwana, ni lini tulikuona mwenye njaa nasi tukakupa chakula, au ukiwa na kiu nasi tukakunywesha maji?

38. Ni lini tulikuona ukiwa mgeni nasi tukakukaribisha, au bila nguo nasi tukakuvika?

39. Ni lini tulikuona ukiwa mgonjwa au mfungwa nasi tukaja kukutazama?

40. Mfalme atawajibu, Kweli nawaambieni, kila kitu mlichomtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi.

41. “Kisha atawaambia wale walio upande wake wa kushoto, Ondokeni mbele yangu enyi mliolaaniwa! Nendeni katika moto wa milele aliotayarishiwa Ibilisi na malaika wake.

42. Maana nilikuwa na njaa nanyi hamkunipa chakula; nilikuwa na kiu nanyi hamkunipa maji.

43. Nilikuwa mgeni nanyi hamkunikaribisha; nilikuwa mgonjwa na mfungwa nanyi hamkuja kunitazama.

44. “Hapo nao watajibu, Bwana, ni lini tulikuona ukiwa na njaa au kiu, ukiwa mgeni au bila nguo, ukiwa mgonjwa au mfungwa, nasi hatukuja kukuhudumia?

45. Naye atawajibu, Nawaambieni kweli, kila mlipokataa kumtendea mambo haya mmojawapo wa hawa wadogo, mlikataa kunitendea mimi.

46. Basi, hawa watakwenda kwenye adhabu ya milele, lakini wale waadilifu watakwenda kwenye uzima wa milele.”

Mathayo 6:20-21

20. Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba.

21. Maana pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.

Muhubiri 12:13-14

13. Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana ndivyo impasavyo mtu.

14. Kwa maana Mungu ateleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri. Likiwa baya.

KUSHIRIKI HABARI YAKO NJEMA

Sehemu Muhimu katika Matembezi yako mapya ni kushiriki Imani yako na wengine. Kila wakati Kumbuka kwamba matendo yako, tabia yako na maneno yako yote yatashuhudia. Kuwa mtauwaa jinsi unavyo weza na tendana na watu na tabia kama ya Kristo. Ha uwezi kulazimu watu, wala kuwashurutisha. Yote unayohitaji ni kushiriki na kuruhusu Mungu afanye kazi. Nawe sasa una ushahidi jinsi amekuja maishani mwako na kubadilisha. Iwapo una fursa ya kuongea na mtu kuhusu Yesu, basi hapa pana mistari ya kusadia kushiriki Injili katika njia fupi lakini yenye uweza.

Warumi 3:23

23. **Watu wote wametenda dhambi na wametindikiwa utukufu wa Mungu.**

Warumi 6:23

23. **Kwa maana mshahara wa dhambi ni kifo; lakini zawadi anayotoa Mungu ni uzima wa milele katika kuungana na Kristo Yesu, Bwana wetu.**

Warumi 10:9

9. **Kama ukikiri kwa kinywa chako kwamba Yesu ni Bwana na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka wafu, utaokoka**.

Ufunuo wa Yohana 3:20

20. Sikiliza! Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi. Mtu akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia nyumbani kwake na kula chakula pamoja naye, naye atakula pamoja nami.

Tafadhili andika katika nafasi iliyo tupu katika ukurasa huu wa kata shauri,
iwapo una kata shauri mpya, au, unafanya upya nadhiri zako. Tunapenda tusikia toka kwako, hata kukuandikia, kuhimiza jinsi umekata shauri kuingia katika jamii ya Mungu. Tupo hapa kujibu maswali na kusaidia katika matembezi yako. Anwani za mawasiliano zipo hapo chini.
AGANO LA KUKATA SHAURI
Tarehe hii, (siku)_____ (mwezi)_____ (mwaka)_____ ,

(Majina yako rasmi) Mimi, _____ Nina kata hili shauri kumkubali wewe, Yesu Kristo, kama Bwana na Mwokozi wangu. Nakuja kuyatoa Maisha yangu kwako, ili uniongoze, unitie nguvu na uniponye magonjwa yangu. Ninapo kosa kufuata njia zako kikamilifu, naomba unionyeshe dhambi, ili kwamba nika tubu hapo na hapo na nikaendelee kuishi kwa haki mbele Yako siku zote za maisha yangu. Nani fanya agano Nawe kufuata amri Zako na moyo wangu wote, nafsi, nia na nguvu zangu, maana umenipenda na ukatoa maisha yaka kwa ajili yangu. Nita kupenda na nita kuabudu. Nina chagua kujifunza toka Kwako kwa kusoma Neno Lako na kushirikiana na watu Wako. Nina chagua kutimia wakati wote Nawe katika maombi kila siku,ili nikujue wewe sawasawa. Amina

Nchi Ya Uganda wasiliana na:
Rev. Lawnsome Etum-Akezi
Christian Communication Centre
P. O. BOX 72 , Lira - Uganda
Tel. +256-473-20637 (office): +256-773-44408 (mobile/ RUNUNU)

Nchi Ya Kenya wasiliana na:
Rev. Julius Ashiono Muteshi
P. O. BOX 764, Bungoma, code 50200, Kenya
Tel. +254-733-868851 au +254-721-339833 au ya nyumba +254-733-902605
Barua pepe: revashiono@yahoo.com

Katika nchi Ya Amerika wasiliana na:
Lenta Hall

P. O. BOX 731
Kamiah , ID 83536
Tel +1-208-935-0602
Barua pepe /EMIAL :

lenta53@myfam.com

Mchungaji Na Dada. Kirby & Linda James
P. O. BOX 731Plum, TX 78952Tel +1-979-242-5439